



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHU



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA

09 Octoba, 2023

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi anapenda kuwatangazia wakazi wote wa Wilaya ya Bahi wenye nia ya kufanya kazi za ajira ya muda (Vibarua) kwa nafasi ya kukusanya mapato katika vijiji vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bahi.

1.0 SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe ni Mtanzania na ni mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, mwenye umri usio pungua miaka 18 na usio zidi miaka 45.
2. Mwombaji awe amehitimu kidato cha IV na kupata Cheti cha matokeo (School Certificate).
3. Mwombaji awe amepitia mafunzo ya taaluma yoyote katika ngazi ya kuanzia astashahada na kuendelea, wenye fani ya kodi, Biashara, Uhasibu, Mipango ya Jamii, n.k. (Watapewa Kipaumbele).
4. Awe na uwezo wa kutumia kompyuta au simu janja.
6. Awe na wadhamini 3 ambao ni lazima wawe watumishi wa Serikali au wanaotambulika vyema katika jamii ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Bahi.

1.1 KAZI ZA KUFANYA

1. Kukusanya Ushuru unaotokana na mazao ya Mimitu, Mazao mchanganyiko, Madini Ujenzi (Mchanga, Kokoto, Mawe) katika Kijiji ambacho atapangiwa ndani ya Wilaya ya Bahi.
2. Kuwalisha fedha Benki iliyotokana na makusanyo hayo kila siku.
3. Kufanya usuluhishi wa kibenki katika PoS.

1.2 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

1. Maombi yapitishwe kwa watendaji wa vijiji/Kata kudhibitisha uhalali wa mhusika.
2. Muombaji aambatanishe nakala za vyeti vya elimu na taaluma kama ilivyo elekezwa hapo juu. Kitambulisho cha taifa NIDA, Picha mbili (Passport size za hv karibuni),

pamoja na barua ya wadhamini ambao ni lazima wawe ni watumishi wa Serikali au watu wanao tambulika katika jamii ya Halmashauri ya Wilaya ya Bahi.

3. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 15/10/2023 saa tisa na nusu Alasiri.
4. Mwombaji asiye fuata maelekezo haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye nafasi ya kufikiriwa kuitwa kwenye usaili.

Maombi yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili/Kiingereza fasaha kuwasilishwa kupitia masijala ya wazi makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bahi au yatumwe kupitia anuani ifuatayo;

**Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Bahi,
S.L.P 2993,
BAHI.**

Imetolewa Na:-


ZAINA M. MLAWA

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHU**

Nakala: Mbao za matangazo & Mitandao ya Kijamii (Facebook&Instagramu)
BAHIDC, Halmashauri ya Wilaya ya Bahi

Tovuti ya Halmashauri (www.bahidc.go.tz)